Gazeti la kwanza la Islam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Na simamisha Sala katika sehemu mbili za mchana na nyakati za usiku (zilizo karibu na mchana). Hakika mema huyaondoa maovu. Huo ndio ukumbusho kwa wakumbukao. (**Huud** 11:115)

JUZU 81 No. 224 | DH.QAD-DH.HIJ 1442 AH | JULAI 2021 | WAFA 1400 HS | BEI TSH. 500/=

Makhalifa Walioongoka - Hadhrat Umar ibn Al-Khattab[ra] na Ensaiklopidia Mpya ya Ahmadiyya

Na **Mwandishi Wetu**

Katika hotuba ya Ijumaa ya tarehe 02/07/2021; Baada ya Tashahhud, Ta'awwudh na Surat Faatihah, Khalifa Mtukufu V, Hazrat Amir ul Momeniin, Mirza Masroor Ahmad[atba] ('Ayyadahullahu Ta'ala Bi-Nasrihil Aziiz') alisema kwamba ataendelea kuangazia matukio kutoka maisha ya Hadhrat Umar[ra].

Khalifa mtukufu[atba] alisema kwamba wakati Hazrat Umar[ra] alipowashinda Wakristo na watu wa asili ya Kiyahudi wa Yemen, hakuwanyang'anya ardhi zao, badala yake alizinunua.

Khalifa mtukufu[atba] alisema kuwa katika Kurani Tukufu, Mungu Mwenye Enzi anasema:

'Haimpasi Nabii kuwa na wafungwa wa vita mpaka apigane vita ya umwagaji damu ardhini. Mnataka vitu vya dunia, hali Allah Anataka Akhera, (8:68).



Tovuti mpya ya AhmadiPedia yenye injini ya utafutaji ambayo inawezesha taarifa mbalimbali ikiwemo za kihistoria kutafutwa kwa urahisi.

Kwa kuzingatia aya hii, Khalifa mtukufu[atba] alisema kuwa Khalifa wa Pili[ra] amethibitisha kwamba Uislamu hauruhusu kumfanya mtu yeyote kuwa mfungwa kando na wakati wa vita.

Wakati mmoja kikundi kutoka Yemen kilikuja kwa Hazrat Umar[ra] na kusema kwamba walikuwa wamefanywa wafungwa katika ardhi yao na Wakristo. Hazrat Umar[ra] alisema kwamba atachunguza, na ikiwa hii itakuwa kweli, hakika angewatoa katika kifungo hicho.

Khalifa mtukufu[atba] alisema kuwa Khalifa wa Pili[ra] (Hadhrat Muslih Mauud), alilinganisha hili na Ulaya ambapo utumwa uliendelea hadi karne ya 19, wakati Uislamu ulikomesha aina zote za vifungo na utumwa karne nyingi zilizopita.

Khalifa mtukufu[atba] alisema kuwa mara moja wakati wa Hazrat Umar[ra], njaa iliikumba Madina na maeneo ya karibu, kwa kiwango ambacho mwaka huu ulijulikana kama "Mwaka wa Majivu". Wakati huo, Hazrat Umar[ra] aliandika barua kwa gavana wa Misri, Hazrat Amr bin Aas[ra] akiomba kupatiwa msaada. Hazrat Amr bin Aas[ra] alijibu kwa kusema kwamba atatuma msafara wa ngamia, kwa kiwango ambacho ngamia wa kwanza atakuwa Madina na ngamia wa mwisho kwenye mstari bado atakuwa Misri. Vivyo hivyo, gavana wa Iraq na Syria pia alituma msaada. Kila wakati misaada ilipowafikia,

Endelea uk 11

Maisha ya Mtume Mtukufu Muhammad[saw]

Yalivyosimuliwa na Hadhrat Mirza Bashir ud Din Mahmud Ahmad r.a.

Khalifatul Masih wa pili wa Masihi Aliyeahidiwa[as]

Inaendelea Kutoka toleo lililopita

KUSILIMU KWA HADHRAT UMAR[ra]

Katika zama hizi hizi kukatukia tukio moja lililowasha moto huko Makka na tukio lenyewe lilikuwa hivi kwamba, Umar[ra] ambaye baadae akaja kuwa Khalifa wa pili wa Islam na katika zama za mwanzo za Islam alikuwa ni miongoni mwa maadui wakubwa (wa Islam). Siku moja alikuwa ameketi na kujiwa na wazo moyoni kwamba hadi sasa jitihada nyingi sana zimefanywa za kuifuta Islam lakini hakuna mafanikio yoyote, kwa nini asiuawe mwanzilishi mwenyewe wa Islam na kuifutilia mbali fitina hii daima dawamu.

Lilipomjia tu wazo hili alinyanyua upanga na kutoka nje ya nyumba na kuanza kumtafuta Mtume[saw] Njiani akakutana na rafiki yake fulani naye akashangaa kumuona Umar[ra] katika hali ile naye akamuuliza waenda wapi ewe Umar? Umar akajibu: Naenda kumuua Muhammad[saw]. halafu



akamwambia je waweza kusalimika na kabila la Muhammad[saw] baada ya kumuua Muhammad[saw]? Hebu kwanza pata habari za nyumbani kwako, hata dada yako na shemeji yako wameshakuwa Waislamu!

Habari hii ilianguka kama umeme juu ya kichwa cha Hadhrat Umar[ra] Akawaza kwamba mimi niliye adui mkubwa sana wa Islam, mimi ninayekwenda kumuua Muhammad[saw], dada yangu mwenyewe na shemeji yangu wameshaukubali Uislamu? Kama ndivyo hivyo basi ni lazima kwanza niwashughulikie dada yangu na shemeji yangu. Alipokuwa akiwaza haya akaelekea nyumbani kwa dada yake. Alipofika mlangoni akazisikia toka ndani sauti nzuri za maneno fulani yakisomwa. Aliyekuwa akisoma alikuwa ni Khubbaab[ra] aliyekuwa akiwafundisha Kurani dada yake na shemeji yake.

Umar[ra] akaingia mle nyumbani kwa kasi. Khubbaab[ra] aliposikia sauti ya ujio wa nyayo za Umar[ra] mara moja akaenda kujificha katika kona fulani ya nyumba na dada yake aliyeitwa Fatima, akazificha zile kurasa za Kurani Tukufu zilizokuwa zikisomwa wakati ule. Hadhrat Umar[ra] akaingia chumbani kwa hasira na kuuliza: Nimesikia kwamba ninyi mmeachana na dini yenu. Baada ya kuyasema haya akaanza kumshambulia shemeji yake ambaye alikuwa pia ni mtoto wa baba yake mdogo. Fatima[ra] alipoona kwamba kaka yake Umar[ra] yu karibu kumshambulia mumewe,

Endelea uk. 3

Buriani Omari Bishazo uk. 4

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

MFUNGE FARASI...

Katika Islam kuna matayarisho kabambe ya kupata kizazi kilicho bora na kitakachokuwa na uwezo wa kuendeleza yale tunayoyathamini na kuyaenzi ambayo ni kutimiza wajibu wetu kwa Allah na viumbe wake. Katika mchakato huo mzima dira inayotuongoza ni nuru ya taqwa - Kuweka matumaini yetu yote kwa Allah kwani bila ya msaada wake na mapenzi yake, bidii zote hizo zitakuwa kama mtu yule anayejaribu kulima jangwani. Havuni wala hatavuna.

Unapotaka kufanya jambo lolote ni busara kujitupa kwenye kizingiti cha Allah kuonyesha udhaifu wako, kumuomba msaada Wake ili Akupe burhani katika jambo unaloliendea. Zipo njia nyingi zinazoweza kutumika ili kuvuta msaada wa Allah kwa mathalan kufunga saumu, kuongeza ibada za nafal, kuendelea kumsalia Mtukufu Mtume Muhammad*saw* Kwa mnasaba huo wa kujenga kizazi bora, tunakumbushwa ya kwamba binti huolewa kwa sababu nne: mali, uzuri, ukoo au dini. Tumeshauriwa kuchagua huyo mwenye sifa ya dini maana yake ana malezi mema yaliyopambwa kwa ua la taqwa. Na siku hiyo ya ndoa nyote wawili mnakumbushwa wajibu wenu. Mnakumbushwa taqwa. Aya zile mbili zinazosomwa siku ya ndoa ni ujumbe tosha wa kurutubisha ndoa yenu. Mnakumbushwa kuwa na *qaulan sadida* – kauli njema. Mnakumbushwa kuwa nyote mko sawa kwani mmeumbwa kutoka nafsi moja isipokuwa majukumu yenu tu ndio tofauti. Mnapokutana pia mnakumbushwa kuomba ili mtoto atakayepatikana awe na mwelekeo wa kumuabudu Allah. Akishazaliwa adhana na iqama inatolewa kwenye masikio yake mawili ikimpa baraka kuwa neno la kwanza sikioni mwake ni mwito kwa Allah. Baada ya siku kidogo hufanyiwa hakika. Jitihada zote hizi zinafanyika za kumlea kwa maadili mema. Anapokuwa kidogo anapelekwa chuoni. Anapelekwa shuleni. Wajibu wako wa lazima unakuwa umeutimiza. Kwa kiwango cha kuridhisha unakuwa umemfunga farasi wako.

Lakini nyumbani kwako sio mwisho wa dunia na wala sio kisiwa. Wapo majirani ambao huna uwezo nao. Ipo shule ambako hufundishi. Kuna wanafunzi wanaotoka mashariki wengine magharibi, wana hulka na mienendo yao, hawa wote mwanao anakutana nao. Pia kuna magazeti, mitandao, ilimuradi mtoto anabaki kutembea kwenye barabara yenye miiba.

Ni kwenye barabara hiyo ya miiba ambako kunatakiwa msaada wa Allah. Hakuna mwenye uwezo huko. Hakuna fundi.

Mtoto wa Nabii Nuhu*as* hakusikia aliyoambiwa juu ya mafuriko na baba yake. Akajidanganya kwa kusema *"nitakimbilia mlimani"*. Siku hiyo hapakuwepo milima.

Ni dhahiri basi, kwamba kila kitu kina mchungaji wake na huyo mchungaji ataulizwa alichopewa kuchunga. Allah Atatizama alivyotimiza wajibu wake. Hataulizwa mwingine. Si mjomba wala shangazi. La msingi kila mtu atimize wajibu wake. Ajitahidi kufunga farasi wake. Tukishamfunga barabara na kuchukua hatua zote za kuhakikisha usalama wake, yaliyobaki yote tuyaweke mikononi mwa Allah.

Siku ya Ukhalifa Mbeya Mjini

Kwa fadhili za Allah maadhimisho ya Siku ya Ukhalifa Tawi la Mbeya Mjini yalifanyika siku ya tarehe 30/05/2021. Maadhimisho hayo yaliyofanyika Makao Makuu ya Kanda ya Mbeya Mjini, Masjid Nasir, yalianza muda mchache baada ya Sala ya alasiri, ambapo Diwani wa kata ya Itiji alikuwa ndiye mgeni rasmi katika maadhimisho hayo.



Ufunguzi wa Maadhimisho hayo ulifanywa kwa usomaji wa Qur'an tukufu iliyosomwa na Mwl Makarani Hamza Balama, ikifuatiwa na usomaji wa Shairi juu ya Ukhalifa lililosomwa na Mwl Nadhiru Ramadhani Deo.

Mada ya Bishara zilizotolewa na Masihi Aliyeahidiwa juu ya Kupatikana kwa Ukhalifa baada yake, iliwasilishwa na Raisi wa Tawi la Mbeya mjini ndugu Munibullah Marunda ikiwa ndiyo mada ya Kwanza katika maadhimisho hayo. Sehemu kubwa ya mada hiyo ilibebwa na nukuu za maandiko ya Masihi Aliyeahidiwa mwenyewe zipatikanazo toka kitabu cha Al Wasiyya ambamo kwa muhtasari Masihi Aliyeadiwa alieleza kuwa ni kawaida yake Allah kuonesha kudra mbili ili kuzifutilia mbali furaha mbili za bandia za wapinzani. Ya kwanza ni kwa kumleta Nabii wake, hapo hupatikana dhihirisho la kwanza la kudra yake kupitia Nabii wake. Pili ni wakati ule ambapo Nabii hufariki, kwa kawaida huwa ni wakati ambao huonekana kuwa bado Jamaat zao hazijapata uimara wa kutosha na kwa vile muasisi wake amefariki basi kwa vyovyote Jumuiya aliyoianzisha nayo itakufa na katika hali hii hata waaminio huanza kupata wasiwasi mioyoni mwao kwa kuhofia itakuwaje, na hapo ndipo Allah mtukufu huidhihirisha Kudra yake ya pili ambayo ni Khilafat.

Mada ya mwisho katika hafla hii ilitolewa na Sheikh wa Kanda, Maulana Karim uddin Shams Sahib. Kupitia mada hiyo Sheikh Karimuddin Shams kwanza kabisa alidokeza juu ya Kutimia kwa Bishara za Ujaji wa Masih aliyeahidiwa na Imam Mahdi, na kubainisha kuwa Ukhalifa Ni zao la unabii na kwamba khalifa ni Kama Naibu wa Nabii ambae hushika nafasi baada ya Kufariki kwa Nabii.

Aidha Sheikh Sahib, kupitia nukuu za Masihi aliyeahidiwa alielezea Sifa hasa za Makhalifa.

Na kwamba kwa kuzingatia vigezo vipi tunaweza kuutambua Ukhalifa hasa ule ambao Mtume s.a.w alitubashiria juu ya Kupatikana kwake, kwa kulingana na Ahadi ya Allah ndani ya Qur'an.

Hotuba hiyo pia ilidokeza juu ya huruma na mapenzi makubwa ya Makhalifa wa Masih aliyeahidiwa kwa waaminio na wanadamu kwa ujumla, moja ya dalili madhubuti kuwa viongozi hawa ni dhihirisho hasa la kudra ya Allah na kwamba kweli wamewekwa na Allah.

Kuihusu nukta ya kuisambaza mafundisho ya Islam na kuwa mfano mwema wa kuwafikishia ujumbe wa amani watu wote Duniani, Maulana Sheikh Shams Sahib alielezea matukio kadha ya juhudi za Hadhrat Khalifatul Masih wa Zama kuwafikishia ujumbe viongozi mbalimbali wa Dunia.

Aidha Sheikh Sahib alielezea jinsi ambavyo Ukhalifa umekuwa sababu ya maungano na umoja hasa baina ya waaminio, kwani kupitia Kiongozi (Khalifa) wetu wa zama ambae hutoa hotuba zake kwenye matukio mbalimbali hususan hotuba ya Sala ya Ijumaa, waaminio na Duniani Kote hupata nafasi ya kusikia maelekezo yake kupitia njia mbalimbali za mawasiliano zilizopo katika zama hizi.

Kwa ujumla Hotuba hiyo iligusa nukta nyingi muhimu na kwa lugha na njia nyepesi kwa mtu yeyote kuweza kuelewa nini maana ya Ukhalifa na Ile shani iliyomo ndani ya Uongozi huu adhwim, ambao daima husimamishwa na Allah Mtukufu mwenyewe.

Kwa kuhitimisha Maadhimisho hayo zawadi za mahitaji ya nyumbani, zilitolewa kwa majirani wa msikiti wetu, hususan zile familia zilizo katika mazingira magumu kiuchumi. Jumla ya familia 20 zilinufaika na zawadi hizo Alhamdulillah. Jumla ya watu 146 walihudhuria maadhimisho hayo.

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Ahmad Abdul Nasibu.
Mchapishaji: Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Maisha ya Mtume Mtukufu Muhammad saw

Kutoka uk. 1

basi akakimbia na kusimama mbele ya mumewe. Umar ra alikuwa ameshaunyanyua mkono na mkono wake ulikuwa unakuja kwa nguvu sana usoni kwa shemeji yake na sasa kuuzuia mkono ule kulikuwa nje ya uwezo wake. Lakini sasa, mbele ya mkono wake, kulikuwa na uso wa dada yake badala ya ule wa shemeji yake. Mkono wa Umar ra ukatua kwa nguvu sana usoni kwa Fatima ra na damu zikaanza kutoka puani mwa Fatima ra

Fatima ra alipata kipigo lakini hata hivyo alisema kwa ushujaa kabisa: Umar ra! Habari hii ni ya kweli kwamba sisi sote tumeshakuwa Waislamu na ukumbuke kwamba sisi hatuwezi kuiacha dini hii, fanya chochote uwezacho.

Umar ra alikuwa ni mtu shujaa. Dhulma haikuufuta ushujaa wake. Alipoliona jeraha lililosababishwa na mkono wake kwa mwanamke, tena mwanamke mwenyewe ni dada yake, Umar ra akazingirwa na aibu na majuto. Damu ilikuwa inavuja usoni kwa dada yake, lakini sasa hasira ikawa imeshaondoka ndani ya moyo wa Umar ra Alikuwa anatamani sana kumuomba msamaha dada yake na hakikumjia kisingizio chochote cha kufanya hivyo. Ndipo akamwambia (dada yake): 'Hebu leteni kurasa zile mlizokuwa mkisoma hivi punde nizisikie.' Fatima akasema sintokuonyeshazo kwani utazichana chana. Umar akasema hapana dada, sintofanya hivyo hata kidogo. Fatima akamwambia: Wewe umenajisika, kwanza nenda kaoge halafu ndipo nitakuonyesha. Majuto yalimsababishia Umar ra awe tayari kufanya kila kitu kiasi ya kwamba akawa tayari hata kuoga.

Aliporejea baada ya kuoga, Fatima akampatia kurasa zile za Kurani Tukufu. Kurasa hizo za Kurani Tukufu zilikuwa na baadhi ya aya za Sura Twaaha. Alipokuwa akizisoma na kufika kwenye aya hii:

Kwa yakini Mimi Ndiye Allah, hakuna aabudiwaye ila Mimi, basi wewe pamoja na wenzako mjumuike na muistawishe ibada yangu, sio tu ibada ya hivi hivi, bali ibada ya kustawisha utakatifu Wangu duniani, na msimamishe Sala kwa kunitaja. Kumbuka kwamba saa ya kustawi kwa maneno haya inakuja, Ninaumba nyenzo za kuidhihirisha ambayo matokeo yake yatakuwa hivi kwamba kila nafsi itapata malipo sawa na itendavyo (Twaha: 15-16).

Hadhrat Umar ra alipofika kwenye aya hii akajikuta akitamka; Maneno haya ni ya ajabu na yaliyotakasika namna hii!?! Khubab ra alipoyasikia maneno haya, akatoka kule alikokuwa amejificha na kusema: Haya ni matokeo ya dua ya Mtume saw Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu kwamba jana tu nimemsikia akiomba dua hii; Ewe Mwenyezi Mungu! Mwongoze mmoja katika mwongozo kati ya Umar bin Khatwaab r. au Umar bin Hisham (Abu Jahal). Hapo Umar ra akasimama na kusema: Niambie Muhammad saw yu wapi.(124 third line bottom)

Alipoambiwa kwamba yeye saw anaishi Darul Arqaam basi akawasili huko akiwa vile vile na upanga mkononi uliochomolewa kutoka kwenye ala na kugonga mlango. Masahaba wakachungulia kwenye nyufa za mlango na kumuona Umar ra akiwa amesimama na upanga uliochomolewa kwenye ala ukiwa mkononi. Wakahofu isije kwa kuufungua mlango Umar akaingia ndani na kuleta tafrani ya aina fulani. Lakini ni nini alichosema Mtume saw! "Fungua mlango!"

Umar ra akaingia ndani akiwa vile vile bado ameushikilia upanga. Mtume saw akamsogelea na kumuuliza: 'Ewe Umar! umekuja kwa dhamira ipi?' Umar akajibu, 'Ewe Mtume wa Allah, nimekuja kuwa mwislamu.' Mtume mkarimu alipoyasikia hayo akapaza sauti akisema 'Allahu Akbar' (Mungu ni Mkubwa kuliko wote) na wale wote wengine waliokuwepo pamoja naye, nao pia wakapaza sauti kwa kutamka yale aliyoyatamka Mtume saw kiasi ya kwamba sauti zao zikavuma na kurusha mwangwi kwenye milima ya Makka na ndani ya muda mfupi tu habari hii ikaenea kama moto mjini Makka. Na Umar naye pia akaanza kusumbuliwa kama walivyokuwa wakisumbuliwa masahaba wengine hapo kabla. Lakini Umar yule yule ambaye mwanzoni alikuwa akiburudika kwa kupiga na kuua sasa akawa anaanza kupata burudanikwa kupigwa. Umar mwenyewe anasimulia hivi kwa kusema: "Baada ya kuamini nikawa napata tu vipigo ndani ya mitaa ya Makka."

Kutengwa Na Kususwa Kwa Waislamu

Kwa uchache dhulma sasa ikawa inavuka mipaka. Watu wengine walikwisha ikimbia Makka na wale waliobakia wakawa ndio mawindo ya dhulma zaidi kuliko ile ya awali. Lakini mioyo ya wadhalimu ikawa bado tu haijapoa. Walipoona kwamba mioyo ya waislamu haikutishika na dhulma zetu za hapo nyuma, mtikisiko haukutokea ndani ya imani zao, bali wakawa ndio wanazidi kumuabudu Mungu Mmoja na chuki yao ya masanamu ikiwa inazidi kuendelea, basi wakaandaa mkutano mwingine wa mashauriano na uamuzi huu ukatolewa kwamba Waislamu watengwe kabisa, mtu yeyote asinunue chochote toka kwao, mtu yeyote asifanye nao biashara.

Wakati huo, Mtume saw na wafuasi wake wachache pamoja na mkewe na watoto na baadhi ya jamaa zake wachache ambao ingawa hawakuwa waislamu lakini hawakuwa tayari kutengana naye, wakalazimika kuchukua hifadhi kwenye nyumba iliyokuwa peke yake iliyokuwa ikimilikiwa na Abu Twaalib. Ilikuwa haiwezekani kwa wanadamu wengine kukisia namna walivyoishi katika zama zile za shida wale watu waliokuwa hawana fedha wakati huo, waliokuwa hawana nyenzo yoyote wala hazina zingezowasaidia kuishi.

Mazingira haya yaliendelea kwa takriban miaka mitatu na uamuzi ule wa watu wa Makka wa kuwatenga haukulegalega hata kidogo. Takriban miaka mitatu baadae ukibuka uasi wa uamuzi ule wa dhulma ndani ya mioyo ya watu wema fulani watano hivi. Wao walienda kwenye mlango wa Shaab Abi Twaalib na kuwaita kwa sauti wale waliokuwa wametengwa humo kwa kuwaambia watoke nje na wao wako tayari kabisa kuuvunja ule mkataba wa kuwatenga.

Abu Twaalib, aliyekuwa anadhoofika kutokana na kutengwa na kususiwa kule kwa muda mrefu, alitoka nje na kuanza kuwalaumu watu wa kaumu yake kwamba yawezaje kujuzu dhulma hii ya muda mrefu kiasi hiki.

Ghafla upinzani ule wa watu wale wema watano ukasambaa mjini kama umeme. Asili ya ubinadamu ikaanza tena kuinua kichwa chake. Roho ya wema ikapumua tena kwa mara nyingine na watu wa Makka wakalazimika kuuvunja mkataba ule wa kishetani.

Mkataba ukawa umekwisha lakini harubu ile ya miaka mitatu ikaanza kuonyesha athari zake. Ndani ya siku chache tu mke mwaminifu wa Mtume saw, Hadhrat Khadija ra akafariki kutokana na shida zile za miaka mitatu ya kutengwa na kususwa na mwezi mmoja baadae, Abu Twaalib naye akaaga dunia.

Vikwazo katika mahubiri baada ya vifo vya Hadhrat Khadija ra na Abu Twaalib na safari ya Taif ya Mtume saw

Itaendelea toleo Lijalo

Sikukuu ya Ei'd ul Adh-ha yafana Jamia Ahmadiyya



Jamia Ahmadiyya Tanzania
Morogoro

Kwa rehema za Mwenyezi Mungu na Baraka za Khilafat,wanafunzi na wakufunzi wa chuo cha Jamia Ahmadiyya hapa nchini pamoja na familia zao,waliungana na wanajumuiya wote nchini na duniani kote kusali na kusherehekea sikukuu ya Ei'd ul Adh-ha mnamo siku ya Jumatano tarehe 21/07/2021.

Sala ya Ei'd iliongozwa na mkuu wa chuo, Maulana Sheikh Abid Mahmood Bhatt sahib katika viwanja vya Jamia-Kihonda Morogoro.

Katika hotuba yake ya Ei'd ,Maulana sahib aliwakumbusha wanatawi matukio ya kihistoria yaliyojiri katika zama za Hazrat Ibrahiim as na mwanawe Hazrat Ismail as na kuzingatia somo lililomo katika matukio hayo ,na kwamba sisi pia ni wajibu wetu kuiga mifano mizuri ya watawa hao.

DHABIHU

Kwa fadhli za Allah,kwa mara ya kwanza katika historia ya chuo chetu cha Jamia Ahmadiyya Tanzania ,kila mwanatawi alishiriki kwa namna moja au nyingine katika kutoa dhabihu.

Wanafunzi walishirikishwa angalau kuchangia ili kuwapa uzoefu wa kujitolea dhabihu wawapo matawini

Jumla ya mbuzi waliochinjwa kama dhabihu ni 29,baadhi ni kutoka makao makuu na baadhi walitolewa na wanatawi kwa kujitolea .

Kati ya mbuzi hao waliochinjwa ,nusu walichinjwa siku ya Ei'd mara tu baada ya sala na wengine walichinjwa siku ya pili ya Ei'd.

MGAO WA DHABIHU

Nyama ya dhabihu iligawiwa kwa kada mbalimbali kama vile wanafunzi, wakufunzi na wafanya kazi wa Jamia, waalimu na wafanya kazi wa shule ya msingi ya Ahmadiyya, majirani, masikini na wasiojiweza, Askari wa usalama barabarani, madereva bodaboda, Wafanyakazi na waathirika wa dawa za kulevya n.k

Zaidi ya hayo, ujumbe wa chuo chetu cha Jamia ulitembelea ofisi za taasisi mbalimbali za umma kwa shabaha ya kugawa zawadi hiyo ya Ei'd. Jumla ya zawadi zilizogawiwa ni zaidi ya 200 na wanufaika wa zawadi hizo walitoa shukrani nyingi na kupongeza Jumuiya ya waislamu kwa utaratibu mzuri wa kuwakumbuka wahitaji katika siku za furaha hizi na kuomba kuwa waendelee na mwenendo huu mzuri.

Taarifa ya shughuli hizi zote ilirushwa katika mitandao mbalimbali ya kijamii.

Buriani Omari Bishazo



Na Mahmood Hamsin Mubiru
Kiwalani Migombani,
Dar es salaam

Ile siku ya Ahadi
Aloipanga Wadudi
Kwako imekuwa budi
Samiina wa atwaana.

Umeitika Omari
Wito wa Mola Kahari
Upokewe kwa sururi
Mapenzi na muawana.

Kila penye upungufu
Akunusuru Latifu
Rabi mwenye Utukufu
Msamehe ya Rabana.

Ni ijumaa asubuhi, saa moja. Tarehe 23/07/2021. Naambiwa Ahmad Bishazo yupo nje ananiita. Natoka chumbani. Nje akiwa ameshika simu yake ya mkononi. Anaponiona tu anatoa Assalaam Alaikum. Nami namuitikia Waaleykumsalaam Warahmatullah wabarakaatuh. Kwa sauti iliyojaa huzuni ananieleza; baba mdogo amefariki. Nataka niwe na uhakika. Nauliza Kabaka? Anajibu ndio. Huku nikitamka 'Innalillaahi wa inna ilaihi raajiuun. Kuna kiti hapo nje na huku nikitokwa na machozi ninapata nguvu kidogo. Nayauliza machozi mbona unadondoka. Yananijibu; ameondoka mtu mwema, mwenye jazba na mapenzi ya Jamaat Ahmadiyya, mkarimu ajabu kwa wageni, anayetanguliza dini mbele ya dunia. Mtu jasiri asiyeficha imani yake. Mwenye bidii na ubunifu katika kutafuta riziki. Mshauri mwema kwa wanaotaka ushauri. Huyo ni Omar Bishazo – maarufu kwa Lakabu ya Kabaka. Aliyefariki tarehe 23/07/2021 katika hospitali kuu ya Mkoa wa Kagera na kuzikwa na umati wa waombolezaji kijijini kwao Katoma kilometa chache kutoka Bukoba Mjini siku ya Ijumaa tarehe 23/07/2021. Kwa hakika sisi ni wa Allah na Kwake tutarejea.

Umati uliojitokeza wakiwemo watu wa matabaka yote ni ushahidi tosha wa wema na matendo aliyokuwa nayo kwa watu. Ilikuwa ni desturi ya Omar Bishazo kufika kila palipo na tatizo na kuwasalimu, kubadilishana nao mawazo bila ya yale majivuno ambayo kwa bahati mbaya wanayo wale ambao wana kipato kizuri zaidi. Majivuno ni jambo ambalo hakuwa nalo asilani nakumbuka nilipoonana naye kwa mara ya mwisho kijijini pake Katoma alikuwa anatoka shambani akiwa na upanga wake mkononi na viatu vile vya kazi akinielezea gharama kubwa ya matibabu iliyopo hivi sasa kwa wenye kipato kidogo. Bila shaka wanapata shida alieleza. Huku tukimsikiliza mimi na bw. Abdu Bishazo na Mwalimu Yusuf Gesonko. Alitueleza juu ya umuhimu wa kuwa na bima ya matibabu. Ili kukabiliana na tatizo hilo. Ni dhahiri yeye alikuwa na kipato kizuri lakini kilichomgusa ni ule moyo wake wa kuwafikiria wasio na uwezo. Ni wachache wenye moyo wa kufikiria maumivu ya wengine. Ni dalili za kuzingatia mafundisho ya Islam kama yalivyowekwa katika vitendo na Mtukufu Mtume Muhammad (saw). Tunalo somo kubwa katika hilo. Kuhubiri uzuri wa Islam haitoshi ni lazima kwa vitendo tuoneshe ubora na usahihi wa mafundisho hayo.

Kwa zaidi ya miaka 40 nimemfahamu Omar Bishazo, wakati huo nikiishi Msikitini Masjid Salaam – Dar es salaam. Kila alipokuja kwa biashara zake kituo chake cha kwanza kilikuwa ni Masjid Salaam. Mara nyingine akiongozana na bw. Habibu Kichwabuta. Tutakaa naye akitueleza mahubiri yanavyoendelea huko Bukoba. Kila alipotoa maelezo hayo uliweza kuona mapenzi yake na bashasha juu ya Jamaat Ahmadiyya. Nakumbuka siku hizo Khalifatul Masih –IV; Hadhrat Mirza Tahir Ahmad (rh) alitoa mubahala dhidi ya adui mkubwa wa Ahmadiyya aliyekuwa Rais wa Pakistan wakati huo –Ziaul Haq. Maelezo ya mubahala yalikuja katika Kiingereza na bw. Omar Bishazo akaniomba nitafsiri mubahala huo katika Kiswahili ili akausambaze huko Bukoba. Yeye tayari alikwishakata tiketi ya basi ya siku mbili baadae akaniomba nifanye haraka na nikalie kazi hiyo bila kutoka. Na akawa ananiagizia chakula palepale ili nisipate usumbufu wa kutoka wa kwenda na kurudi. Nilifanya kazihiyo usiku na mchana. Ikapigwa mashine na akaenda na vipeperushi ambavyo vilitawanywa kwa wingi mjini Bukoba. Na kila paliposhambuliwa Jamaat alifanya kila njia ya kujibu mashambulizi kwa hoja na dalili. Kwa Omar Bishazo uguse kitu chochote kile lakini sio Jumuiyya yake ya Ahmadiyya. Nakumbuka kuna kipndi alifunga safari kutoka Bukoba kuja Dar es salaam ili kukamilisha safari ya kwenda London –U.K kwenye mkutano mkuu wa Jalsa Salana. Yalitokea matatizo fulani kuhusu Waingereza. Kwa hiyo hakuweza kusafiri kwenda huko. Hata hivyo hapana shaka yeye alipata haki sawa na hadithi ya kwanza ya Mtume (saw) iliyomo kwenye kitabu maarufu cha hadithi *Sahihi Bukhari* isemayo kwamba; 'Innal amal biniyyat' (Kila tendo huhesabiwa kwa nia yake).



Marehemu Omari Bishazo (mwenye kanzu na kofia yenye bendera ya Tanzania katikati) akiwa na Watanzania wenzake katika Jalsa Salana ya Uganda Januari 2020

Juu ya mapenzi yake juu ya Jamaat, dr. Kitabu alinikumbusha juu ya tukio la Omar Bishazo kumfuata katika mvua iliyokuwa inanyesha mtu aliyechukua mali fulani ya Jamaat. Alimshika shati akaja naye mpaka Msikitini. Na akamwambia mali ya Jamaat haichezewi.

Ninaposoma habari za Nabii Ibrahim[as] katika Qur'an Tukufu inanikumbusha ukarimu mkubwa na mapenzi ambayo Nabii Ibrahim alikuwa nayo kwa wageni wake. Omar Bishazo alijitahidi sana katika kuwakaribisha wageni na bil khususi wageni wa Jamaat Ahmadiyya. Hapo miguu haikanyagi chini. Ni pilika pilika panda shuka. Na utamuona fikra zote zimeelekeza katika kuwahudumia.

Wakati wa kumbukumbu ya miaka 50 toka kufariki kwa mwandishi mahiri wa Kiswahili Shaabani Robert, kongamano la kumbukumbu hilo lilifanyika mkoani Kagera. Lililoratibiwa na mshairi Abdallah Msakanjia. Wataalamu wa Kiswahili waliohudhuria ni pamoja na Profesa Mlokozi na Dr. Mtembei. Jumuiyya ya Ahmadiyya ilikaribishwa rasmi kutokana na ukarimu iliokuwa nao na Shaabani Robert. Bw. Amir Kaluta na mwandishi wa makala haya tuliteuliwa kuwasilisha mada katika kongamano hilo. Tulituma habari hizo Bukoba. Ninaambiwa na wale walio karibu na bw. Omar Bishazo ya kwamba siku hizo walimuona akishughulika sana mpaka wakamuuliza hao wageni waheshimiwa wanatarajiwa lini? Ilikuwa ni furaha na mapenzi ya ajabu aliyotuonesha bw. Omar Bishazo. Tayari mahali pa kulala na chakula vilikuwa vimetayarishwa. Huduma zote za usafiri na chakula alizibeba kwa shauku kubwa na mapenzi. Sheikh Durani wakati huo akiwa Amir na Mbashiri Mkuu alitembelea Kagera na kushuhudia wema, mapenzi na ukarimu wa Omar Bishazo. Amir wetu wa sasa Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry naye anaeleza moyo wa mapenzi na kujitoela aliomuonesha yeye na ujumbe wake alipotembelea Bukoba. Wale waliohudhuria Jalsa ile maarufu ya Uganda 2021 wanakumbuka makaribisho tuliyoyapata tuliposimama kwa muda msikitini Katoma na kupata dhiafat ya kukata na shoka. Kwa hakika Bishazo wote bw. Abdu, bw. Yahya, bw. Yakubu na bw. Omar wana utamaduni wa ukarimu na hiyo yote ni katika kutimiza 'Ruhumaa bainahum' (Waaminio ni wenye kuhurumiana wao kwa wao).

Kuhusu sala ya ijumaa, Allah Anahimiza juu ya sala hiyo. Na kuwaambia watu waache biashara na waende misikitini kuabudu. Biashara ina mtihani mkubwa. Ina vishawishi vingi. Unaona nikitoka unayemdai atakuja sasa hivi. Dakika moja ya kupoteza inakufanya kuumwa na kichwa. Mfanyabiashara anapenda kila

Inaendelea uk. 5

Buriani Omari Bishazo

Kutoka uk. 4

wakati awe anahesabu. Hataki kutoka kwenye biashara zake. Ni kujitolea muhanga kutoka kwenye biashara. Biashara zote za Omar Bishazo zilikuwa Bukoba Mjini. Kilometa chache hadi Katoma. Panamwendo. Nahukondikokuna msikiti wa Jamaat Ahmadiyya. Ni ijumaa na biashara imechanganya vizuri. Unafanyaje. Hapo ni kuchinja nafsi. Inayokuamrisha uendelee na biashara. Uruhusu ile nafsi lawama ikusukume uende ukasali ijumaa. Omar Bishazo alishinda mtihani huo. Akiwa yupo Bukoba na hayupo nje ya Bukoba kwa biashara zake basi hakosi Ijumaa. Atawapakia watoto wake na kuhudhuria sala ya Ijumaa. Tabia ya kuwabeba watoto ni ya msingi kwani unawapa ujumbe watoto juu ya umuhimu wa sala ya Ijumaa. Sio kwa maneno bali kwa matendo. Na hakuna jambo linaloheshimiwa katika Islam kama kutenda yale unayoyaamrisha. Ni chukizo kinyume cha hivyo. Kama anavyosema Allah; Mnaamrisha mema na kusahau nafsi zenu. Omar Bishazo katuachia somo la kuepuka kumkasirisha Allah. Nakumbuka katika miaka ya 1980 Sheikh Muhammad Munawwar akiongozana na aliyekuwa Katibu Mkuu wa Jumuiyya Muhammad S. Kibindu walihangaika sana katika kupata fedha za kigeni wakati huo Sheikh Muhammad Munawwar alikuwa akielekea Nigeria alikokuwa amehamishiwa kikazi. Siku hizo kupata fedha za kigeni ilikuwa shughuli pevu. Walifika benki kuu wakitarajia kupata msaada kutoka kwa Ahmadiyya aliyekuwa pale. Kwa masikitiko makubwa hawakupewa msaada. Yule aliyetegemewa kutoa msaada alijificha pengine kuogopa asifahamike imani yake pale benki. Lakini kinyume chake bw. Omar Bishazo pamoja na kuwa biashara zake zilizoshamiri mjini Bukoba, lakini hakuwa na tabia hiyo ya kuficha imani yake. Mara zote yeye alijisikia fahari kupata ndugu zake wa kiroho na daima alitoa kipaumbele kuwahudumia. Tunapata somo kubwa hapo alililotuachia bw. Omar Bishazo kwamba kila mmoja wetu analo jukumu na dhima ya kuhakikisha anabakisha alama ya kukumbukwa kwa wema, mahali popote alipo; ikiwa ni mfanyakazi au mfanyabiashara kila mmoja anayo fursa ya kulingania imani yake na kubakisha alama kwa ajili ya funzo kwa ndugu wa baadae. Tukifanya hivyo tutakuwa tumepiga ndege wawili kwa jiwe moja. Yaani tutapata baraka za kutanguliza dini juu ya dunia. Tukumbuke ule mfano wenye athari kubwa kwa mioyo kutoka kwa Mtukufu Mtume Muhammad^{saw} wakati huo akiwa bado kijana. Siku moja alipomuona bibi kizee mmoja amebeba mzigo mkubwa yeye alimhurumia na kumuomba ampokee mzigo wake. Wakati huo haikuwepo desturi kama hiyo ya kuwasaidia wenye uhitaji. Bibi yule walipofika mwisho wa safari kwa namna ya kulipa ihsani aliyofanyiwa, alimueleza kijana wangu mimi sina cha kukulipa kwa wema ulionifanyia, lakini napenda nikuonye jambo moja tu kwamba jihadhari na mtu mmoja wa hatari sana ambaye anatoa madai ya ajabu ajabu na kuwapoteza watu. Hapo kijana yule akamuuliza; huyo mtu anaitwaje ili nimfahamu?, akamjibu anaitwa Muhammad. yule kijana akasema bali mimi ndiyo Muhammad. Yule bibi alishtuka! Na kusema wewe ndiye Muhammad? Mara moja yule bibi akakiri na kusema; ikiwa wewe ndiye Muhammad basi mi ninakuamini na kuthibitisha madai yako yote ni ya kweli. Jiwe moja kwa ndege wawili. Kila mmoja wetu anayo fursa ya kulenga shabaha sawasawa ili daima tupate faida maradufu kwa kutanguliza dini juu ya dunia.

Kumbe inawezekana kabisa kutafuta riziki halali, ukafanya biashara kwa uadilifu, ukachakarika ukatoa jasho ukiwa umetawaliwa na hofu ya Allah. Inawezekana kabisa shughuli zako zote ikawa ni ibada. Kwa sababu umeitafuta riziki kihalali na unaitumia kihalali. Na inaleta manufaa kwa binadamu. Omar Bishazo alijitahidi sana kutafuta riziki halali. Hakuchoka. Alifanya kazi kwa bidii na ufaulu wake haukumfanya abweteke. Aliendelea kubuni mbinu mpya za biashara na katu hakutaka kupoteza muda. Aliyakumbuka sana maneno ya Masihi Aliyeahidiwa, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad^{as} ya kwamba muda wangu hautapotezwa. Ni siri ya mafanikio ambayo aliitumia vizuri Omar Bishazo na sisi tuige mwendo huo.

Kwa vyovyote itakavyokuwa, kifo kinatukumbusha kuwa kuna siku tutaondoka. Qur'an inatukumbusha; 'Kila nafsi itaonja mauti'. Mtu ambaye kila mara anakumbuka mauti yake hawezi kuweka matumaini yake katika maisha haya wala katika mali yake au madaraka yake. Hivi vyote tutaviacha na tutakachokwenda nacho ni taqwa. Taqwa ndiyo itakuwa nuru yetu tukishakufa. Tunamuomba Allah Ampatie nuru hiyo Omar Bishazo na sisi sote tuombe maombi yaliyomo katika Qur'an Tukufu; "*Mola wetu ututimizie nuru yetu, na utughofirie, hakika Wewe ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu*". (66:9)

Kutoka Viwanja vya Maonyesho ya Sabasaba



Kwa msaada wa Allah mwaka huu Tanzim yetu ya Khuddamul Ahmadiyya Tanzania tulipata bahati ya kushiriki katika maonyesho ya 45 ya sabasaba 2021 kwa kutoa huduma katika banda letu la Jamaat sabasaba. Tulikuwa na vitabu mbalimbali, Kiswahili aina 98, Kiingereza aina 109, Kiarabu aina 55, Kiurdu aina 27 na pia tulikuwa na tafsir za Quran Tukufu katika lugha zipatazo 57 ikiwemo Kiswahili na Kiyao.

HUDUMA:

Timu ya wahudumu 11 ilitoa huduma tangu tarehe 28/06/2021 mpaka mwisho wa maonyesho tarehe 13/07/2021 katika banda letu ambalo ni banda pekee lenye huduma za mafundisho sahihi ya Dini ya Islam, vitabu vya aina zote vyenye kutimiza haja nzima ya maisha ya mwanadamu, maswali mbalimbali yaliyokuwa yanawatatiza watu juu ya mafundisho ya Islamu yalijibiwa na wataalam wetu waliobobea juu ya elimu ya Dini. Kubwa lililokuwa gumzo ni juu ya ujaji wa Masihi na Nabii wa za hizi Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s ambapo picha yake kubwa iliwekwa mbele ya jengo letu na kuleta mvuto wa kipekee kwani hapo ndipo zilipokuwa zikianzia mada, watu wengi waliipenda picha hiyo na kutaka kujua na wengine walikuwa wakipiga picha na familia zao katika picha hiyo kubwa ambapo ujumbe wa "Masihi Aliyeahidiwa Ameshafika" ulikuwa chini yake.

Mbali na huduma hizo za kiroho tuliweza pia kutangaza huduma mbalimbali za kijamii zinazotolewa na Jamaat kama vile; Shirika la kibinadamu la Humanity First, shule za awali, msingi na sekondari, Hospitali ya Morogoro, Muslim Television Ahmadiyya (MTA), Radio Ahmadiyya, Printing Press, na huduma za ujenzi wa Misikiti Nchini.

WAGENI:

Tarehe 04/07/2021 Amir na Mbashiri Mkuu, Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry alitembelea Maonyesho ya Sabasaba ambapo alipokelewa kama kiongozi mkuu wa Jamaat nchini, na viongozi wa TANTRADE pamoja na Khuddam wetu waliokuwa wakitoa huduma



Amir na Mbashiri Mkuu pamoja na ujumbe wake katika picha ya pamoja na Mkurugenzi wa TANTRADE

Endelea uk 10

Bustani ya Washairi

YAKINI

Kikombe kimetakata, kwa nje kinavutia
Kwa kila anayepita, mate anakimezea
«Na mimi ningekipata, fuadi ingetulia»
kumbe siri ya maiti, aijuae muosha!

Pamwe na mshika kata, maji anayemwagia
Kimya huwa anasita, lolote kujisemea
Kila mpenda kubwata, kichwani zimepungua
Akatula omungoma, kamanywa omubambi

Uzuri wenye kumeta, ni ndani kuchungulia
Yaliyomo ni mafuta, au uchafu ajaa
Bila yakini tajuta, katika hino dunia
Tizama nje na ndani, kuupata utulivu

Kaditama hujapata, bileshi wajisumbua
Yakubidi kujikita, kiini kukifikia
Au utaula mwata, janga utajivunia
Na kila mvuna janga, hula pamoja na wake

Mahmood Hamsin Mubiru (Wa Mamba)
Kiwalani - Migombani

Ndugu Walotangulia, Dua Tunawoambea

1. Ya Ilahi ya Manani, Mpweke tangu na tangu
Ardhini na mbinguni, wang'arisha ulimwengu
Mmiliki kila shani, nani Akukwepe Mungu
Naombea ndugu zangu, Ya Rabbi uwaauni

2. Amekwenda Nuruddin, poleni kina Mnungu
Katupotea machoni, bado twaona ukungu
Lakini tufanye nini, nasi sote ni wa Mungu
Naombea ndugu zangu, Ya Rabbi uwaauni

3. Ali mpole moyoni, mvumilia machungu
Tuli naye ofisini, kutafuta uchamungu
Ya Rabbi Umuauni, ling'arishe lake fungu
Naombea ndugu zangu, Ya Rabbi uwaauni

4. Kaaga dokta Mwanga, akiwa Mbeya nyumbani
Ali bingwa wa uganga, aso kiburi moyoni
Alojitoa muhanga, kuhubiri mitaani
Malalo ya kaburini, Mola wawashie mwanga

5. Mwanzoni alijiunga, kumwitika Muadhini
Mipaka akaichunga, hakuwajali wahuni
Akautibu ujinga, na magojwa miilini
Malalo ya kaburini, Mola wawashie mwanga

6. Kweli alikuwa mwanga, mwenye taa mkononi
Majukumu hakuchenga, kizazi na majirani
Udugu aliuchunga, wa damu na wa imani
Malalo ya kaburini, Mola wawashie mwanga

7. Katuondoka Daudi, machozi yatiririka
Kwa Molawe amerudi, twabaki kusikitika
Kama mshindo wa radi, kwa hofu tumeshtuka
Wabaki kusitirika, hawa wajao Wadudi

8. Alianzia Devidi, lakini hakutosheka
Kwa moyo wake baridi, mwisho akasalimika
Kwa wema wako Wadudi, mipaka akaivuka
Wabaki kusitirika, hawa wajao Wadudi

9. Ujumbe wake Mahadi, kwake ulipomfika
Hakufanya ukaidi, wito akauitika
Idara ya Jaidadi, kwa yeye ikapambika
Wabaki kusitirika, hawa wajao Wadudi

10. Kaenda zake Masamba, Allah mfanye apae
Juzi tulivuta kamba, tukiwa pamoja nae
Leo yu kwako Muumba, kweli dunia kigae
Hawa uwaghufirie, Ya Ilahi twakuomba.

11. Wala hakuwa mwembamba, mwili mnene ajae
Ila mbingu ikipamba, jambo gani tushangae
kama macho kuyafumba, ghafla uyafumbue
Hawa uwaghufirie, Ya Ilahi twakuomba.

12. Kwa wema bila kuvimba, sauti aisikie
Ndani ya Masihi nyumba, haraka ajikalie
Akaukwepa ushamba, 'Isa mbinguni apae'
Hawa uwaghufirie, Ya Ilahi twakuomba.

Sheikh Abdulrahman M. Ame

HADAA ZA WANAWAKE:

1. Yahitaji umakini, na subira nyingi sana
Hata kama una dini, kukosa Sala hakuna
Ni maua ya chumbani, ila ‹siamini sana
Hadaa za wanawake, kusumbua wanaume.

2. Ila siamini sana, hata wale wa shambani
Kugusana ni hapana, utazama maungoni
Hata kama wamenona, siwatazame machoni
Hadaa za wanawake, kusumbua wanaume.

3. Siwatazame machoni, dhambi utazitafuna
Tuwaweke migongoni, ili tusiweze ona
Nawakumbusha jamani, wala siongei sana
Hadaa za wanawake, kusumbua wanaume.

4. Eti kuna urafiki, mwanaume mwanamke
Tusilete unafiki, tusijepata maseke
Mungu tusimdhihaki, sicheze na mwakamke
Hadaa za wanawake, kusumbua wanaume.

5. Sicheze na mwanamke, hata kama una laki
Atakufanya Bushoke, hatakama hautaki
Waulize wa Temeke, wanatembezwa mswaki
Hadaa za wanawake, kusumbua wanaume.

6. Usilete itifaki, kwa mambo wa wanawake
Wewe jifanye konki, huko ndani wakusweke
Kule hupatikaniki, huku mefanywa udeke
Hadaa za wanawake, kusumbua wanaume.

7. Kuwa makini kijana, duniani mitihani
Usipige dana dana, ukaribie ndoani
Uache kugandamana, na sumu za kiunoni
Hadaa za wanawake, kusumbua wanaume.

8. Hawa viumbe jamani, wala ‹sishindanenao
Silete upunguani, na watu wa muambao
Utabebwa mgongoni, takua kalagabao
Hadaa za wanawake, kusumbua wanaume.

9. Huyu huyu mwanamke, ishi nae kwa akili
Ni lazima mkumbuke, wana mioyo miwili
Ngoja siku acharuke, utaona mbili mbili
Hadaa za wanawake, kusumbua wanaume.

10. Ila kwa ufupi sana, usiwaamini kamwe
Ukiona sina mana, tafakari kwali mmwe
Kwa nyakati za mchana, hawapendagi watumwe
Hadaa za wanawake, kusumbua wanaume.

Abdallah Kalindima (K-mtoto)
#MMAKONDE MSOMI

UZURI HASA

Kwa jina Lake Kahari, ndilo ninalotamka
Anijalie khairi, niweze kueleweka
Niifikishe khabari, pale panapotakika
Uzuri hasa ni kitu, au wa mtazamaji?

Kitu hupata uzuri, ukawa wa kusifika
Na tena ulo dhahiri, pote pote unawaka
Hakika unaathiri, na pia hauna shaka
Uzuri hasa ni kitu, au wa mtazamaji?

Kama chakula sukari, utamu inasifika
Ailaye hudhihiri, hii tamu ya hakika
Utamuwe huathiri, ulimi husisimka
Uzuri hasa ni kitu, au wa mtazamaji?

Huwa hanayo habari, homa inapomshika
Kuwa ni tamu sukari, mdomoni ikifika
Moyo wake ukihiri, na mara huitapika
Uzuri hasa ni kitu, au wa mtazamaji?

Mtume mwenye fakhari, Muhammadi katamka
Husuda tujihadhari, wemani tutaondoka
Sababuni kama nari, kwenye kuni ikishika
Uzuri hasa ni kitu, au wa mtazamaji?

Muhamad kadhihiri, ushahidi uso shaka
Na kwa mengi matabiri, vitabu vya kablika
Vilieleza dhahiri, ni Nabii wa Rabuka
Uzuri hasa ni kitu, au wa mtazamaji?

Japo Mola Kahari, Kasema ni msifika
Vitabu vimekariri, ni mkweli aso shaka
Lakini watu jeuri, tafakuri likakuka
Uzuri hasa ni kitu, au wa mtazamaji?

Hoja wakatahayari, kukosa la kutamka
Wakaipanga shari, ya mauti kumfika
Ikabidi ahajiri, Madina kutoka Maka
Uzuri hasa ni kitu, au wa mtazamaji?

Ndivyo alivyodhihiri, Ahmad kwa hakika
Ushahidi wa Bukhari, Muslim kadhalika
Quran yakariri, Manabii watafika
Uzuri hasa ni kitu, au wa mtazamaji?

Yeye kwa kudhihiri, dini imeimarika
Bidaa zilokithiri, zenyewe zinatoweka
Ya Muhamadi athari, inabidi kung›arika
Uzuri hasa ni kitu, au wa mtazamaji?

Twangalie kwa ari, husuda kuiepuka
Ndio hasa kwa dhahiri, wema wetu hufunika
Tukashindwa jua siri, Nabii aliyefika
Uzuri hasa ni kitu, au wa mtazamaji?

Tumuombe ya Kahari, Mola Aliyetukuka
Atujuze hiyo siri, ya Nabii Msifika
Na tena Atusitiri, tukubali pasi shaka
Uzuri hasa ni kitu, au wa mtazamaji?

Hassan Sango (Jange Muqadas, kwenye karatasi)
Dar es salaam

KIZAZI_TEULE

Ni kizazi teule, Kijukuu cha sahaba
Kilo vikwa usukule, Kwacha ya dini mahaba
Kilo sahau ya kale, Kumbu ni visa nasaba
Siye warithi wa Yule, Masihi muahidiwa

Neema nyingi hulevya, Hula nguvu ya maombi
Rohoni Uja huavya, Kumfanya mja zombi
Salani huanza chovya, ndipo hugeuka pimbi
Zisitulevye laghui, Na anasa za dunia

Shunda Mshudia wana
Daluni, Tanga

DAWA

Mambo yakikulemea, usipoteze wakati
Kutwa kiguu na njia, kwa wale wasaka noti
Si waganga nakwambia, haja yao sharubati
Dawa nenda kwa Molao, upate tiba kamili

Mahmood Hamsin Mubiru (Wa Mamba)
Kiwalani - Migombani

JIUNGENI NAMI

Mie jua la Baraka, Sayari nizungukeni
Na kwenu sina Mipaka, Mpatapo nizuruni
Na msipo bahatika, Kwa barua sabahini
Kwa waso elimika, Niwekeni sujudani
Ni sauti iitayo, Upande wa Ukhalifa
Shunda Mshudia wana
Daluni, Tanga

Nabii Suleiman[as] na Kijana

Allah alimteremshia wahyi Nabii Sulayman[as] akimuamrisha kutembelea ufuo wa bahari ili kushuhudia nguvu za uwezo wake. Nabii Sulayman[as] alienda na wafuasi wake lakini hakuona kitu chochote cha maajabu.

Kwa hivyo aliamuamrisha jinni kupiga mbizi baharini ili amletee habari za ndani. Baada ya kutoka mle baharini, yule jinni alisema, "Sikuweza kufikia kina cha bahari na wala sikuona kitu chochote cha kueleweka."

Akamuamrisha jinni mwengine ambaye alikuwa na nguvu zaidi ya yule wa kwanza. Jinni huyu wa pili alienda mbizi mara mbili ya kina cha yule wa kwanza lakini hata yeye hakuweza kuleta habari yoyote.

Baadaye akamuamrisha waziri wake mwenye busara, Waziri Shaykh Asif bin Barkhiya Akazama Chini ya Bahari Kwa muda mfupi sana, Asif Barkhiya alileta kuba kubwa jeupe la kafuri lenye milango minne mbele ya mahakama ya Nabii Sulayman[as]. Mlango mmoja ulikuwa umetengenezwa kwa lulu,wa pili kwa yakuti, wa tatu kwa almasi na wa nne kwa zumaridi.

Kuba lenyewe halikuwa na tone hata moja la maji ijapokuwa milango yote ilikuwa wazi. Ndani ya kuba hili kulikuwa na kijana mwenye umbile zuri, aliyevalia nguo safi na maridadi akiwa katika sala. Alipomaliza kuswali, Sulayman[as] akamsalimia na akataka kujua kuhusu siri ya kuba lile.

Akasema yule kijana : "Ewe Mtume wa Allah Baba yangu alikuwa mlemavu na mama yangu alikuwa kipofu . Niliwatumikia kwa miaka sabini. Kabla ya mamangu kufariki aliomba ya kwamba Ewe Allah nakuomba umjaalie mwanangu umri mrefu wa heri."

Babangu kipenzi kabla ya kufariki naye pia aliomba: "Ewe Allah nakuomba umjaalie uwezo mwanangu wa kuabudu mahali ambapo shetani hataweza kumjaribu."

Baada ya kufariki na kuwazika nilikuja katika ufuo huu nikaliona kuba hili nikaingia ndani. Wakati huo huo alikuja malaika na akalipeleka kuba hili mwisho wa kina cha bahari."

Kijana Alipoulizwa na Nabii Sulayman[as] kuhusu muda alioishi mule. Alijibu, "Nimeishi hapa tangu enzi ya Nabii Ibrahim[as]."

Nabii Sulayman[as] alitambua kuwa imempita miaka elfu mbili tangu aingie katika kuba lile na bado angali kijana na hata hakuwa na unywele mmoja mweupe katika kichwa chake! Alipoulizia kuhusu chakula chake alisema: Kila siku ndege wa rangi ya kijani kibichi huniletea kitu cha rangi ya manjano mdomoni mwake nami hukila. Kina ladha ya utamu wote wa duniani. Kinanitosheleza kwa njaa na kiu.

Juu ya hayo nimesalimika na joto, baridi, usingizi, uvivu, upweke, uwoga na vituko. Baada ya hapo, kutokana na ombi la yule kijana na kuamrishwa na Sulayman Shaykh Asif bin Barkhiya ali lichukuwa kuba na akalirudisha ndani ya bahari.

Baada ya haya Sulayman[as] alisema: "Enyi watu, Allah awateremshie rehema zake Je, mumeona jinsi DUA ya wazazi Inavyokubaliwa! Jiepusheni na kuwakosea wazazi wenu."

Bila ya shaka mwenye kufurahisha wazazi wake amebahatika sana. Na yule mwenye kuwakasirisha wazazi wake hakuna kingine chochote (atakachokipata) ila maangamizi.
Na tumeagizwa kuwafanyia wema mkubwa wazazi. Kama mmoja wao akifikia uzee naye yuko pamoja naye au wote wawili basi usiwaambie hata **Ah!** Wala usiwakemee na useme nao kwa msemo wa heshima kabisa.

N.B. Maneno haya: watu na majinni, ambayo yanapatikana katika Aya nyingi za Qur'an, hayaonyeshi viumbe vya namna mbili mbalimbali, bali yanaonyesha watu wa namna mbili. ***Ins*** ni watu wote wa kawaida na ***Jinn*** ni watu wakubwa wasiochanganyika ovyo na watu wengine, na hawaonekani mara kwa mara. Viongozi waovu wameitwa majinni na wafuasi wao ni watu wajinga. Hao wote huwa ni adui za Mitume.

Jinn (viumbe wa siri) ambao, kinyume na Malaika, wao walipewa uwezo wa kutii na kuasi.

CHEMSHA BONGO

Kuna wanyama wangapi katika kila picha?





UNGANISHA NUKTA

Unganisha nukta ili upate picha moja iliyokamilika.



Jinsi ya kupika Samaki wa mayai

Na **Mtandao**



MAHITAJI:

Samaki (Nguru) 1 kilo | Vitunguu. 1 kilo | Tungule (nyanya) 1 kilo | Mayai 6 | Thomu | Pilipili manga | Samli 1/2 kilo | Binzari Nzima | Ndimu | Chumvi.

JINSI YA KUPIKA

Mkate samaki mtie chumvi, pilipili, ndimu umkaange.. akikwiva muweke pembeni.

Kataa vituungu, saga Tungule (nyanya), Thomu na viungo vingine.

Teka sufuria itie samli, ikichemka tia vitunguu mpaka viwe vyekundu. Tia tungule, thomu na viungo vyote. Chukua vipande vyote vya samaki uvitie, kisha tia ndimu na maji kidogo.

Kisha onja, vitu vikiwa sawa anza kuvunja yai mmoja baada ya lingine, tia juu ya samaki bila kuharibu kiinii.

Funika kwa mkungu.. palilia na mto mdogo ili yai lipate kuiva.

Angalia,ukiona imekwiva epua pole pole bila kuharibu mpangilio wa mayai.!

NUKUU YA HADITHI

Na **Ustadhi Issa Malenge** - 0625 914 740 0752 334 332

وعن أَبي العباس سهل بن سَعد الساعِدِيّ رضي الله عنه أَنَّ رَسُول الله صلى الله عليه وسلم بَلَغَهُ أَنَّ بَني عَمرو بن عَوْفٍ كَانَ بَيْنَهُمْ شَرٌّ، فَخَرَجَ رسولُ الله صلى الله عليه وسلم يُصْلِحُ بَينَهُمْ في أُنَاس مَعَهُ، فَحُبِسَ رَسُول الله صلى الله عليه وسلم وَحَانَتِ الصَّلاة، فَجَاءَ بِلالٌ إِلَى أَبي بكر رضي الله عنهما، فَقَالَ: يَا أَبَا بَكْر، إِنَّ رَسُول الله صلى الله عليه وسلم قَدْ حُبِسَ وَحَانَتِ الصَّلاةُ فَهَلْ لَكَ أَنْ تَؤُمَّ النَّاس؟ قَالَ: نَعَمْ، إِنْ شِئْتَ، فَأَقَامَ بِلالٌ الصَّلاةَ، وتَقَدَّمَ أَبُو بَكْرٍ فَكَبَّرَ وَكَبَّرَ النَّاسُ، وَجَاءَ رَسُولُ الله صلى الله عليه وسلم يَمْشِي في الصُّفُوفِ حَتَّى قَامَ في الصَّفِّ، فَأَخَذَ النَّاسُ في التَّصْفيقِ، وَكَانَ أَبُو بكرٍ رضي الله عنه لا يَلْتَفِتُ في صَلاتِه، فَلَمَّا أَكْثَرَ النَّاسُ في التَّصْفيقِ الْتَفَتَ، فإِذَا رَسُول الله صلى الله عليه وسلم، فَأَشَارَ إِلَيْه رسولُ الله صلى الله عليه وسلم فَرَفَعَ أَبُو بَكْر رضي الله عنه يَدَهُ فَحَمِدَ اللهَ، وَرَجَعَ القَهْقَرى وَرَاءهُ حَتَّى قَامَ في الصَّفِّ، فَتَقَدَّمَ رَسُولُ الله صلى الله عليه وسلم، فَصَلَّى للنَّاسِ، فَلَمَّا فَرَغَ أَقْبَلَ عَلَى النَّاسِ، فَقَالَ: ((أَيُّها النَّاسُ، مَا لَكُمْ حِينَ نَابَكُمْ شَيْءٌ في الصَّلاةِ أَخَذْتُمْ في التَّصفيق؟! إِنَّمَا التَّصفيق للنِّساء. مَنْ نَابَهُ شَيْءٌ في صَلاتِهِ فَلْيَقُلْ: سُبْحَانَ الله، فَإِنَّهُ لا يَسْمَعُهُ أَحدٌ حِينَ يقُولُ: سُبْحَانَ الله، إلا الْتَفَتَ. يَا أَبَا بَكْر: مَا مَنَعَكَ أَنْ تُصَلِّيَ بالنَّاسِ حِينَ أَشَرْتُ إِلَيْكَ؟))، فَقَالَ أَبُو بَكْرٍ: مَا كَانَ يَنْبَغي لابْنِ أَبي قُحَافَةَ أَنْ يُصَلِّي بالنَّاسِ بَيْنَ يَدَيْ رَسُول الله صلى الله عليه وسلم. مُتَّفَقٌ عَلَيهِ.

Abdul Abbas Sahl bin Sa'ad*ra* anasimulia kwamba Mtume*saw* alipata khabari ya ugomvi uliotokea kati ya watu wa Bani Amr bin Auf. Mtume*saw* akatoka na kwenda pamoja na baadhi ya Maswahaba kuwapatanisha. Huko alizuwiwa kwa ajili ya kukutana na watu hata wakati wa sala ukafika.

Bilal alimwendea Abu Bakar na kumwambia kuwa Mtume*saw* anezuwiliwa huko na sasa ni wakati wa sala utaweza kusalisha watu?.

Yeye akaitikia na kusema ndiyo, kama ukitaka. Bilal akasoma Iqama na Abu Bakr akaenda mbele na sala ikaanzishwa. Mara Mtume*saw* akafika na kwenda moja kwa moja akipita kati kati ya mistari na kusimama katika safu ya kwanza. Hapo waliokuwa wanasali wakaanza kupiga makofi. Abu Bakr akaendelea kusalisha na hakujali.

Makofi yalizidi naye akamuona Mtume*saw* yuko huko na kwa ishara akamuongoza Abu Bakr aendelee kusalisha.

Lakini Abu Bakr akainua mikono yake na kusema Alhamdulillah akarudi nyuma na kuingia katika safu. Mtume*saw* akasogea mbele na kusalisha.

Sala ilipokwisha alikaa akiwageukia waliokuwa nyuma yake na kuwaambia. Kwa nini nyinyi mnapiga makofi mkiwa ndani ya sala?

Linapotokea jambo fulani kupiga makofi ni kazi ya wanawake tu. Lakini mnapoona jambo lolote limetokea mkiwa ndani ya sala semeni "***Sub,hana llah***" (Allah ni mtukufu). Hiyo itatosheleza moyo.

Na wewe Abu Bakr kwa nini hukuendelea kusalisha hali mimi nilikutolea ishara uendelee? Yeye akajibu: Haifai kwa mwana wa Abu Kahafah kuongoza sala mbele ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu.

(Bukhar na Muslim).

DARASA LA QUR'AN TUKUFU

Hutumii Akili?

Na **Musa Salum Mgeleka -** 0717 504 690

Humpa hekima Amtakaye, na aliyepewa hekima bila shaka amepewa heri nyingi; na hawakumbuki ila wenye akili. (Surah 2:270)

HUTUMII AKILI ni Kauli maarufu kwenye Jamii zetu, Kauli hutumika kukumbusha juu ya Kutumia Akili yake hukumu jambo na bila shaka hutaka kuamshwa kwa Hekima yake iliyolala. Kauli hii ikatafsiriwa tofauti kama tusi kwa sababu hana Hekima hiyo. Kutumia Akili yaani Kutumia HEKIMA Humaanisha maana Tatu hivi sawa na maana ya Hekima ilivyotumika kwenye aya 10:2

1۞ Kutumia Maarifa ya jambo husika,

2۞ Kujiepusha na Laghwi (Upuuzi - Kufanya kwa usahihi, Nyakati sahihi, Mahali sahihi na Hali sahihi) wa jambo husika, na

3۞ Kuhukumu kwa HAKI katika Hitilafu.

Haya yote ni Asili ya binadamu ambayo hayahitaji tofauti kubwa baina yetu na ndio maana hutumika Kauli hutumii Akili kwa yeyote anayetakiwa Kutumia Akili. Asili hii hurudishwa kwa kuwa UKARIMU. Sawa na Maelezo ya Masih Aliyeahidiwa as alivyonukuliwa kwenye Kitabu cha Masharti ya Baiat. Sawa na Aya mbalimbali ikiwemo aya 2:269 Ukarimu huletwa kwa KUJITOLEA na Kujitolea husababishwa na kuwa na Subira, Mkweli/ Haki, Utii 3:18 na Kuacha Dhambi na Kumcha Allah 64:17

Akili isiyo na Ukarimu na Matendo yasababishayo Ukarimu, Akili hufumbwa uwezo wake Kutenda ipasavyo, Akili inaweza kuwa na Maarifa na au Ikajiepusha na Laghwi maana hizi zinasomewa na Kufundishwa ila HAKI ni Asili ya Allah 30:31 na Asili hii haipatikani ila kwa daima kuwa Mwislamu. Mtu mwenye Maarifa hudhani ndiye mwenye Akili na au mwenye Uwezo wa kuepuka Laghwi Anajifaharisha kwa maaridadi wake wa kuendea mambo. Ila bado hatumii Akili. Dunia imejawa Maarifa na Sheria na kanuni za kuepuka Laghwi ila hajaondokana na Hitilafu baina yao. Magomvi, chuki na Hasira zimendelea kutanda duniani ila Quran Tukufu sehemu mbalimbali inaendelea kutunasihi MBONA HAMTUMII AKILI? Jipime Unapoambiwa Huna Akili? Hutumii Akili Hukasirika, Huchukia, Hutukana/ Hugombana? n.k maana ndio Hali ya WANAFIKI walioelezwa katika aya 2:77 na Akiwauliza MHATUMII AKILI? Ukiona hali baadhi hizo zimo ndani mwako tambua AKILI YAKO INAUPUNGUFU SEHEMU FULANI NA HUNA AKILI

Tunamuomba Allah Atujalie Hekima na Atujaze Kheir Zake katika Hekima. Amin

ASEMAVYO MASIHI ALIYEAHIDIWA*AS*

Kudhihiri kwa Mwenyezi Mungu

Mimi nasema kweli kwa hakika kama roho zina hamu ya kutafuta na nyoyo kupata shauku ya elimu, basi hapo wanadamu watapata jazba ya kugundua mwanga ule na Njia ile. Lakini mtu awezaje kuifikia Njia ile na macho yatafumbuliwa namna gani? Nawahakikishia wale wote watafutao ya kuwa ni Islam pekee itoayo habari njema za njia ile. Dini zingine zilishauziba mlango wa wahyi wa Mungu tangu zamani za kale. Hivyo, jueni kwa yakini kwamba si Mwenyezi Mungu Aliyeukwamisha ufunuo. Bali ni mwanadamu, ili kuhalalisha kunyimwa kwake, yeye anafuta kujibanza kwenye kisingizio hiki. Fahamuni wazi (kabisa) kwamba kama vile isivyowezekana kuona pasina macho au kusikia bila masikio au kuongea bila ya ulimi, vivyo hivyo ndivyo isivyowezekana kumwona Mwenyezi Mungu wetu, Mpendwa, bila Qurani Tukufu. Nilikuwa kijana. Sasa nimezeeka. Lakini sikumwona ye yote ambaye, pasina chemchem hii safi ya Qurani Tukufu, akajaaliwa kunywa toka kikombe cha mwongozo ulio safi ujidhihirishao.

(Roohani Khazain Jal. 1, Maelezo Uk. 191-192).

MATUKIO KATIKA PICHA



Mkuu wa Chuo cha Jamia Ahmadiyya Tanzania pamoja na baadhi ya walimu wa chuo na wanajamaat baada ya kugawanya dhabihu tayari kwa kugawiwa siku ya Idi el Adha.



Wanajamaat wa Kikunde katika picha ya pamoja baada ya ibada ya Idi el Adha.



Kipindi cha mazoezi ya viungo kikiendelea katika darasa la Atfal na Nasrat Kaluta House, Magomeni



Sheikh wa Mkoa wa Mbeya pamoja na mgeni rasmi wakikabidhi zawadi kwa mwananchi katika Maadhimisho ya siku ya Ukhalifa



Khuddam waliokuwa wanasoma Dodoma katika vyuo mbalimbali katika hafla ya kuwaaga. Wawili toka Mtwara, mmoja toka Morogoro na mwingine toka Iringa



Khuddamul Ahmadiyya wa Sungamile kabla ya mechi ya kirafiki kuanza.



Khuddam wakiongozwa na Mwl Musa Kaswezi katika Wakal Amal ya kushusha mawe kwa ajili ya ujenzi wa msikiti



Wahudumu wa banda la Ahmadiyya Muslim Youth Association kwenye maonyesho ya Sabasaba wakitoa huduma ya vitabu

Kutoka Viwanja vya Maonyesho ya Sabasaba

Kutoka uk. 5



Amir na Mbashiri Mkuu akitambulishwa wa wahudumu wa banda la Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) alipokuwa akipitishwa.

sabasaba kisha kuonana na mkurugenzi wa TANTRADE na Kufanya mazungumzo machache kisha kusaini Kitabu cha wageni na baadae kukabidhiwa ulinzi na mtu maalum wa kumtembeza katika maonyesho hayo. Miongoni mwa mabanda aliyoyatembelea ni; SIDO, JKT, Mahakama, UDOM, Wamachinga, Wajasiriamali na mwisho akamalizia katika banda letu la Ahmadiyya. Akiwa katika banda letu la Ahmadiyya Amir sahib alipongeza lakini pia alishauri wakati ujao InshaAllah kila idara inayohusika na huduma katika banda letu la Ahmadiyya awepo mwakilishi wake. Wakati wa kuondoka alipitia ofisi za TANTRADE na kuagana na mkurugenzi ambapo mkurugenzi alimshukuru sana kwa huduma zinazotolewa na Jamaat na kusema tunajali uwepo wenu na aliahidi ushirikiano.

Pia tulitembelewa na mwandishi wa habari wa blogu na mtangazaji wa Redio Newala anaitwa Bwana Mbudifo ambaye ana upofu. Lakini pia tuliweza kuhojiwa moja kwa moja na Redio Ahmadiyya Mtwara juu ya maendeleo ya utoaji wa huduma sabasaba kwa huu 2021, hali halisi iliyopo na ni huduma zipi tunazozitoa na nini tunawashauri watu wote waliotembelea sabasaba juu ya Uwepo wetu Ahmadiyya na huduma tunazozitoa.

Ambapo tuliwashauri watu kwa ajili ya kumaliza kiu yao ya Imani kwa kupata majibu ya maswali yote yaliyokuwa yakiwatatiza kuhusu dini yao basi wasikose kutembelea banda adhiim ya Jumuiyya ya waislam Ahmadiyya.

MATUKIO YA KUSISIMUA:

Mama mmoja alirudisha Tafsir ya Quran Tukufu aliyoinunua sabasaba ya mwaka 2019 baada ya Kupata upinzani mkubwa kutoka kwa mmewe na ndugu, alikuwa akiisoma kwa siri na baadaye akahifadhi vizuri alitueleza kuwa yeye binafsi haoni tatizo lolote kuwa na Quran yetu ambayo ni nzuri na inaeleweka vizuri katika usomaji lakini hakuwa na jinsi ndugu na mumewe walimtenga na kumuambia akitaka maelewano yarudi ndani ya nyumba mpaka arudishe Quran aliyoinunua kutoka kwa Waahmadiyya, ndio yule mama alihifadhi vizuri na aliposikia mwaka huu tumeshiriki akaileta kuikabidhi na akasema; kwangu Qurani hii ni nzuri na haina kipingamizi chochote hivyo naitoa kama sadaka, akapewa maelekezo na akashukuru na Quran imehifadhiwa kwa ajili ya kumbukumbu.

Tukio jingine ni mume kumuondoa mkewe katika banda letu baada ya kugundua ni banda la Ahmadiyya na hakutaka kuelekezwa chochote, lakini mkewe hakulizika kwani mkewe alikuwa ana utulivu mkubwa akiuliza vitabu mbalimbali na alinunua Kitabu cha sala, juu ya suala hilo walivutana kidogo mke hakuridhika na kumwambia mimi sioni tatizo.



Muonekano wa banda la Ahmadiyya katika maonyesho ya Sabasaba

Bwana mmoja alipokea vipeperushi vyetu viwili kimoja kina anuani ''Utambulisho wa Jumuiyya ya Waislam Ahmadiyya'' na kingine chenye anuani ya ''Tusiwakashifu viongozi wa dini zingine'' alipotoka tu kuanza kukisoma cha kwanza na kugundua kuwa ni cha Waislam Ahmadiyya akaenda hatua tatu akarudisha cha utambulisho akaondoka hatua zingine tatu aliposoma kingine pia akarudisha baada ya kugundua kile cha pili nacho kina jina Ahmadiyya.

Sheikh mmoja akubali kifo cha Nabii Issa kijanja na kusema subirini nikafanye utafiti kwani Aya hiyo aaah! Watu wakamuuliza unaikataa au unaikubali akasema basi sikatai ngojeni nikafanye utafiti.

Mama mmoja aliona bango la Masihi Aliyeahidiwa katika banda letu lilimshangaza sana kwani yeye anajua habari za Masihi dajal tu na kwa kushawishiwa na mwanaye wa miaka 13 waliingia ndani na yalifanyika mazungumzo kwa takribani dakika 40 akatoka akiwa ameelewa vizuri sana akashukuru na kuahidi kuwa tutaendelea kuwasiliana na alituachia namba zake za simu kwa ajili ya kuendelea kuelimishana.

Bwana mmoja wa kizungu kutoka Australia alikuja kwa nia hasa ya kutupa changamoto, alipokuja alikuwa anaongea bila ya kutupa nafasi kwa mwingine na alipopewa habari za Jamaat akasema, Ahmadiyya naijua sana huko tunakotoka ina harakati kama hizi za kwenu hapa, tulipotaka tumueleze habari hizi vizuri akakataa, lakini baadae alirudi tena kwenye banda letu akiwa mstaarabu kuliko hapo kabla na akasema, jamani msinifikirie vibaya mimi ni mstaarabu niliongea vile ili kuwapa changamoto tu ila nimewakuta mpo imara kuthibitisha mnachoamini, lakini kujadili zaidi alikataa na kusema muda hautoshi ili kuthibitisha ukizingatia nyinyi mnavyo vitabu lukuki vya mafundisho yenu.

Kuna Sheikh mmoja alijitambulisha kwetu kuwa yeye ni mtu wa pemba na Jumuiyya ya Ahmadiyya anaitambua toka zamani lakini kulingana na uchache wa elimu aliyokuwa nae wakati huo hakuweza kuwa na hoja, lakini sasa hivi majuzi tu amerudi toka Oman kusoma mambo ya Dini pia alidai ana shahada ya lugha ya Kiarabu, hivyo alituomba tafsiri ya Kiswahili ya Quran Tukufu na akasema bahati mbaya ameishiwa fedha zote na hiyo anahitaji sana wakati huu kwani kwa elimu aliyonayo anataka kuisoma Ahmadiyya ili kujua ukweli hivyo tulimpatia Zawadi ya Quran Tukufu ya Kiswahili na Kitabu cha uongofu wa tafsiri ya Quran Tukufu, alituachia namba zake za simu na kuahidi kuwa atajitahidi kuwasiliana nasi InshaAllah.

Kuna vijana wanafunzi wa ngazi A level, walistushwa baada ya kuingia katika banda letu na kukuta Kitabu chenye kichwa cha habari ''KAFARA YA YESU'' wakauliza nanyi Waislam mnaamini kafara ya Yesu, wakafahamishwa vema juu ya kafara ni nini na jinsi gani wakristo walivyoanguka kwa kuamini vibaya hiyo kafara ya Yesu wakaelewa vizuri na kufurahi.

Kubwa zaidi katika Tabligh ya sabasaba watu wengi wanapata kuijua Islam Ahmadiyya na mafundisho yake matakatifu, lakini tunapata nafasi ya kujibu tuhuma zote za uwongo ambazo watu wengi wanakuwa wamepatiwa na Maulamaa wapotofu na hatimaye kubainikiwa na ukweli.

Tuligawa vipeperushi elfu kumi (10,000) vyenye ujumbe mbalimbali kama vile; *Utambulisho wa Jumuiyya ya Waislam Waahmadiyya, Tusiwakashifu Viongozi Watakatifu wa Dini Zote, Jiepusheni na Maana Potofu za Jihadi* na *Uislam Hauna Uadui na Ukristo.*

Pia tulipokea maoni ya watu wengi waliotembelea banda letu waliotamani vitabu vingi zaidi viwepo katika mfumo wa sauti ili kumrahisishia msomaji pia vitabu vya zamani viliombwa kudurufiwa tena.

SHUKURANI:

Shukran tele kwa Amir na Mbashiri Mkuu Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry kwa kutuunga mkono na kuliwezesha tukio hili. Pia Sadr majlis Khuddamul Ahmadiyya Tanzania ndugu Rahim Mwanga kwa usimamizi na muongozo wake katika kila hatua.

Pia shukrani za dhati ziende kwa Sadr Sahib Majlis Ansarullah ndugu Ally Mbambwa kwa ushirikiano wake mkubwa alioutoa yeye mwenyewe kwa kujitoa kuhudhuria siku za huduma lakini pia kwa kuweka mwakilishi wa kudumu kutoka Tanzim ya Ansarullah. Allah Awabariki bali Atubariki sote Aamin.

Kwa nini *Biblia Ni Jibu* Wanamkana Nabii Issa kuwa Si Yesu?

Na **Juma Iddy Abeid,** Kigoma

Inaendelea Kutoka toleo lililopita

UTABIRI

Wakiendelea kuhusu Issa wameandika tunaposoma Qurani, hatuoni andiko lolote linalo mzungumzia Kutabiriwa kwa Issa. Hivyo hivyo huyu Issa yeye hakutabiriwa na Nabii yeyote kama Musa , Isaya , Daudi n.k Yesu Ndani ya Biblia kuna tabiri 63 za Manabii walitabiri habari za Yesu kristo. Hebu tuangalie tabir chache katika hizo.

Kwa hiyo Bwana mwenyewe atawapa ishara. Tazama ata chukua mimba atazaa Mwanaume nae atamwita jina lake Imanueli Isaya 7:14 na Isaya 9:6-7mwisho wa kunukuu.

Hoja hoyo mbele yay a kesi ya Issa na Yesu hapo haina msingi kama ni hakimu lazima aombe ushahidi toka kwa wazazi wa mlengwa .kwa mfano ni kweli kabisa ndani ya Qurani na hakuna utabiri wa jina la Issa .

Lakini hata wao hakuna andiko lolote katika Biblia ambalo Mama wa Yesu si wakitabu cha Luka wala Matayo alipata kumuita jina hilo la Imanueli sasa atueleze je wazazi wa Yesu walikua makaidi?

Maana walishindwa kutekeleza utabiri wa makaidi? maana walisndwa kutekeleza utabiri wa kumwita Imanueli kama walishindwa kumwita ndio kusema Yesu akutabiriwa wala issa lasivyo waonneshe katika Injili zote nne wapi Yesu kapewa jina Immanueli ili Issa asiwe Yesu.

UTABIRI AGANO LAKALE

Atakuwa uzao wa Yuda Mwanzo 19:10
Atakuwa mwana wa Mungu Zaburi 2:7
Watu wakuu watamsujudiwa watoto wa watu Yeremia. Akasema Imetimia kwa kunukuu Waebrania 7:14 maana ni dhahiri kwamba Bwana watu alitoka katika Yuda kabla ambayo Musa hakunena neno lolote juu yake mambo ya kuhani.

Ukiona utabiri wa Mwanzo 19:10 *Atakuwa uzao wa Yuda* sasa kama Yesu ni tofauti Issa kwa hoja hiyo na iwe kweli wangeonesha mzazi wa Yesu wa ukoo huo wa Yuda, Issa yeye hana baba na kabila ni urithi toka kwa baba mpaka hapo wamekosa Ushahidi wa kumtenganisha. Issa ni Yesu.

Atakuwa Mwana wa Mungu Zabur 2:7; Inasema Nitahubiri amri. Bwana alinambia , Ndiwe mwanangu , mimi leo nimekuzaa Mwandishi wa Biblia nijibu akadai imetimia katika Luka 1:32-35 huyo atakuwa mkuu ataitwa mwana wa aliye juu atampa kiti cha enzi cha Daudi Baba yake . Atamiliki nyumba ya Yakobo hata milele na ufalume wake utakuwa hauna mwisho.

Watu hao walikuwa waongo kwa kuwadanganya wawaumini wao maana ZABURI 2:7 ilimuhusu Daudi. Daudi ndie aliyeambiwa ndie mwanangu na siku iyo akatarifiwa kuwa leo yani Muda alipoambiwa ndio Amezaliwa . Hapo sio Yesu.

Hata Luka 1:32-35; Ina ushahidi hata wa mfanano kwani Yesu hana Damu ya Daudi atamiliki nyumba ya Yakobo hata milele na ufalme wake hauna mwisho. Ajabu Yesu hakupata kuwa mfalme na alipoulizwa kama Mfalme alijibu ufalme wake si wa dunia hii. YOHANA 18:36;

Ufalme wangu sio waulimwengu huu kama ufalme wangu ungekuwa wa ulimwengu huuwatumishi wangu ungekuwa wa ulimwengu huu watumishi wangu wangeupigania nikatumwa mikononi mwa mayahudi lakini ufalme wangu sio wa hapa .

Nadhani mpaka hapo wameshindwa juthibitisha ndio kusema Yesu wana mtetea kuwa sio Issa vigezo watavyo bado havitoshelezi.

Hizo ni baadhi ya tabiri walizo dai zimetimia kumbe hazikutumia kwa Yesu pia .

WAKAJA NASABA

Kuhusu wazazi wao wakasema; Watu wengi wanaposoma kwa Issa ndiye Yesu husema kwamba kwakuwa mama yake Yesu alikuwa akiitwaa Mariam. Hivyo kwa kigezo hicho Issa ndie Yesu.

Wakasema waandishi hao kua hoja haina nguvu kwani akina Mariam wako wengi. Tatizo si kufanana na majina tatizo ni mariyamu yupi aliye mzaa Yesu na Mariyamu yupi aliye mzaa Issa?

Hapo biblia ni jibu wanaonesaha kuwa wapo mamariam wengi walio zaa watoto bila kuguswa na mwanaume. Hi sema ni kweli kwani Mariyam wa luka alikuwa na mme waketofauti na wa Mariyam wa Matayo kama tulivyo ona mwanzo. Isitoshe wamemuongezea na Mariyam aliye mzaa Issa ambae alikuwa hana mme aliyetajwa na Quran.

Wakiendelea na hoja yao wanajenga kuwa kwa mujibu wa Qurani Mariam alie mzaa Issa ni dada yake na Haruni. Qurani 19:28; *''Ewe dada yake Harun. Baba yako hakuwa mtu mbaya wala mama yako hakuwa asherati''* wakamaliza wakasema Aya hii Inaonesha jinsi watu walivyokuwa wakimshutumu Mariyamu kwa kuzaa watoto ambae baba yake hajulikani hivyo kwa mujibu wa maandiko hayo Mariamu ni dada yake na Harun akatwaa taji mkononi mwake .

Wakajenga hoja kuwa; Huyu Mariyam ambae ndie dada yake Harun yeye alikuwa ukoo wa hawa kwani Haruni na Mussa ni wa ukoo wa hawa na Bwana Yesu alikuwa wa ukoo wa Yuda Zaidi ya hapo Mariyamu ambae alimzaa Yesu hakuwa nabii. Wakati Mariyamu ali mzaa Yesu hakuwa Nabii na huyu Mariyamu aliishi miaka 1500 kabla ya kristo hivyo basi kwa mujibu wa Quran ambayo inasema kuwa Mama yake Issa ni dada yake na Haruni kumbe nikwamba Issa awezi kuwa Yesu kwa sababu Issa aliishi miaka 1500 kabla ya Yesu mwisho wa kunukuu.

Lakini kama nilivyosema awali Yesu kwa kuwa wapo wawili tofauti yani yupo wa Mathayo na wa Luka, *Biblia ni jibu*hawakuonesha wanampinga yupi Bali na habari za Luka na Yohana ambazo za kuingia kwa hao wawili wenye majina ya wazazi wao na walivyo kiasi kwamba hata hao Biblia ni jibu hawa jui wanamuongelea nani na wana mpinga yupi

Taadhari ni kwa waumini maana Yesu alisema kipato akimuongoza kipofu wote wawili wata tumbukia shimoni . Lakini lazima tujue Yesu na mama yake walikuwa wakienda hekaluni ndio kusema mariamu alikuwa mfuasi wa taurati.

Na taurati ni kitabu cha mussa Na Haruni jua hii nae mama yake Yesu aliishi miaka 1500 kabla ya kumzaa mwanae Bila shaka sio hoja .

Ila tujue Taurati inaadhabu kwa wazinifu na watu wlkuwa wakimwona Mariam hana mme ila alikuwa karibu na fundi seremala mmoja na hatimae akajihisi ana mimba . Ikambidi akimbie pale alipo kuwa anaishi ili adhabu ya kupigwa mawe Isimkabili . Stori inaonesha seremara huyo alimuoa ila harusi aikutangazwa kwakua hakuwa mtu maarufu. Je alienda hovyo alienda kwa ndugu yake ?Hila Biblia ni jibu hawakusema sijui wanaona aibu au wqanaogopa kuumbuka ? mimi sijui ila tuone maandiko haya ;LUKA 1:39- Basi Mariyamu hakaondoka siku hiyo (ZA UJAUZITO)akaenda hadi nchi ya milimani kwa haraka mpaka mji mmoja wa Yuda akaingia nyumbani kwa Zakariya akamuamkia Elizabeti.

Huko ndiko aliko kimbiliwa Mariyamu ili asihukumiwe kwa dhana ya kuhalifu amri ya kuto zini .

Sasa hebu tumjue uyu Elizabeti ambaye Mariyamu alienda kupata hifadhi kwake alikuwa nani LUKA 1:5-6; Zamani za Herode mfalme wa wa yaudi palikuwa na kuhani mmoja jina lake Zakaria , wa zamu ya abiya na mkewe alikuwa mmoja wapo wa uzao wa Haruni, jina lake Elizabeti.

Hapo mwandishi aliyejitaftia mambo kwa uswahili anasema Elizabeti alikuwa wa uzao wa Haruni je nay eye Elizabeti alishi miaka 1500 kabla ya Yesu ? jibu hapana.

Tukisoma Luka 1:56- Inasema Mariyamu akakaa nae kadiri ya miezi mitatu kisha akarudi kwenda nyumbani kwake .

Sasa mpaka hapo kazi kwa wenye kutafakari Biblia nijibu walinukuu aya 19:28kuwa Mariyamu ni dada wa Haruni , kumbe ukitizama ni kweli kwani Mariyamu mama wa Yesu na Elizabeti mama wa Yohana mbatizaji ni ndungu wao ni mtu na ami yake kiukoo Yesu alikuwa ana mwita Yohana mbatizaji kaka . Ndio kusema Qurani haina tatizo kwani ushahidi hapo umekamilika nakma sio ndugu vipi akae nae miezi mitatu bila mahusiano ya dam?

Nadhani hata Elizabeti huyu likuwa nyumba ya Yuda na Biblia ni jib undo walipo kuwa wameona ni bora waoneshe Mariyam wa nyumba ya lawi. Wakaacha wa nyumba ya Yuda kwa kutokujua kwa o maandiko au kwa husuda yao ilivyo wapotosha macho.

KIFO CHAKE

Itaendelea toleo lijalo

Makhalifa Walioongoka - Hadhrat Umar ibn Al-Khattab[ra] na Ensaiklopidia Mpya ya Ahmadiyya

Kutoka uk.1

Hazrat Umar[ra] alitoa maelekezo kwamba kwanza wapatiwe wale wanaoishi vijijini. Hazrat Umar[ra] pia aliandaa chakula, na tangazo likawa linatolewa kwa kila mtu ambaye anahitaji chakula aje kuchukua chochote anachohitaji.

Khalifa mtukufu[atba] alisema kwamba wakati fulani chakula kilipowasilishwa mbele ya Hazrat Umar[ra] ambacho kilikuwa na nyama. Aliuliza ni wapi imetoka na akaarifiwa kwamba ilikuwa ni ya ngamia mmoja ambaye alikuwa amechinjwa. Hazrat Umar[ra] alihoji atakuwa kiongozi wa aina gani, ikiwa angejiwekea chakula bora na akawapa wafuasi wake sehemu iliyobaki. Kwa hivyo aliomba kichukuliwe na badala yae aletewe kitu kingine. Imeandikwa kwamba Hazrat Umar[ra] hakula nyama au siagi (katika kipindi hicho cha njaa) hadi kila mtu alipokula vizuri na kurudi katika hali yake ya kawaida. Imeandikwa kwamba rangi ya ngozi yake ilianza kuwa nyeusi kwa sababu ya chakula kidogo alichokuwa anakula.

Khalifa mtukufu[atba] alisema kwamba Hazrat Umar[ra] aliagiza idadi ya watu waliokuwa wanakuja kula inapaswa kuhesabiwa. Ilipohesabiwa, ilibainika kuwa watu 7,000 walikuwa wamekuja kula naye, na siku nyingine idadi hiyo iliongezeka hadi 10,000. Hii iliendelea hadi mwishowe, ambapo kwa maombi ya Hazrat Umar[ra], mvua ilinyesha na njaa ikawa imetoweka.

Khalifa mtukufu[atba] alisema kuwa mwanzoni kwenye misikiti, sala zilisaliwa chini (bila mikeka), kwa sababu hiyo mapaji ya uso ya waliosali mara nyingi yalikuwa yamefunikwa na matope. Imeandikwa kwamba Hazrat Umar[ra] alikuwa wa kwanza kuamuru kwamba mikeka kwa ajili ya kusalia inapaswa kutandikwa chini ili kurahisisha kusali. Ilikuwa pia wakati wa Hazrat Umar[ra] kwamba Msikiti wa Mtume[saw] (Masjid Nabawi) ulifanywa ukarabati na kupanuliwa.

Khalifa mtukufu[atba] alisema kwamba ilikuwa pia wakati wa Hazrat Umar[ra] alipoanza kuchukua sensa ili kujua idadi ya raia, pia ilikuwa wakati huu ambapo Hazrat Umar[ra] alianzisha

Endelea uk 12

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

MapenziyaMungu

DH. QAD - DH. HIJ 1442 AH | JULAI 2021 | WAFA 1400 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu[saw]

"Mtu atakayeomba kama ilivyofundishwa katika Aya mbili za mwisho za Surat-ul-Baqara, basi zinamtosha" (Bukhari). Tena imesimuliwa, "Mtume[saw]. alipoomba kwa maombi haya, akaambiwa katika kila tamko, 'Imefanywa'." Na Mtume[saw]. akasema. "Allah Ameteremsha aya hizi mbili toka hazina za Peponi." (Baidhawi).

Makhalifa Walioongoka - Hadhrat Umar ibn Al-Khattab[ra] na Ensaiklopidia Mpya ya Ahmadiyya

Kutoka uk. 11

mfumo wa mgao wa chakula kwa kaya. Hii ilikuwa ni kwa mujibu wa usawa ule ule ambao ulianzishwa na Mtukufu Mtume[saw] mara tu alipofika Madina. Wakati mmoja wakati wa vita, Mtukufu Mtume[saw] aligundua kuwa watu wengine hawakuwa na chakula cha kutosha, wakati kulikuwa na wengine ambao walikuwa na chakula kingi. Kuona hivyo, Mtukufu Mtume[saw] aliagiza kila mtu ambaye alikuwa na kitu cha kula akikusanye, na kisha kikagawanywa sawa ili kila mtu aweze kula. Kwa kawaida kila mtu alikuwa anakula chakula chake kando kivyake kwa muda wote ilipowezekana kufanya hivyo, lakini wakati hatari ya wengine kubaki na njaa ilipoibuka, Mtukufu Mtume[saw] aliagiza kwamba wote wanapaswa kula sawa. Khalifa mtukufu[atba] alisema kuwa hii haikumaanisha kuanzisha ujamaa wowote au ukomunisti, bali ni uamuzi uliofanywa kulingana na mazingira ya wakati huo. Kwa hivyo, huu ndio mfano uliowekwa na Mtukufu Mtume[saw].

Khalifa mtukufu[atba] alisema kwamba ni kwa kuzingatia mifano iliyowekwa na Mtukufu Mtume[saw], kwamba wakati Uislamu ulipoanza kuenea mbali na mataifa mbalimbali yakaanza kujiunga na Uislamu, kwamba Hazrat Umar[ra] alianzisha mfumo wa kuhesabu watu katika kujua idadi ya raia, na kisha kusambaza chakula chini ya mfumo wa mgao wa kaya ili kuhakikisha kuwa wale wote wanaokuja kwenye zizi la Uislam waliweza kupata chakula. Kwa hivyo, serikali ya Kiislamu ilianzisha mfumo, ambao riziki ya kila mtu ikawa jukumu la serikali. Inasemekana kuwa Soviet-Urusi ilikuwa ya kwanza kutoa mahitaji kwa raia wake baada ya kuchukua sensa. Walakini ni ukweli uliothibitishwa kuwa dhana hii ilianzishwa kwanza na Uislamu na serikali yake.



Hadhrat Khalifatul Masih V[atba] akiongoza maombi ya kimya baada ya kuzindua tovuti ya AhmadiPedia

Khalifa mtukufu[atba] alisema kwamba wakati wa Hazrat Umar[ra], nchi ziligawanywa katika majimbo ili kusaidia kuwezesha shughuli za kiutawala. Vivyo hivyo, ilikuwa wakati wa Hazrat Umar[ra] ndipo mfumo wa Shura (mashauriano) ulianzishwa. Ilikuwa wakati wa mikutano hii ya mashauriano kwamba mawaziri wa idara tofauti na magavana wa maeneo tofauti walikutana. Hazrat Umar[ra] alianzisha sheria na miongozo fulani kwa wasimamizi wa ofisi, ili kuhakikisha kuwa hawaangukii kiburi au mapenzi ya dunia. Ilikuwa pia wakati wa Hazrat Umar[ra] kwamba ushuru ulifanywa kuwa rahisi zaidi ili kuwawezesha raia kulipa.

Khalifa mtukufu[atba] alisema kwamba ataendelea kuangazia maisha ya Hazrat Umar[ra] katika hotuba za Ijumaa zijazo.

Mwishoni mwa hotuba yake, Khalifa mtukufu[atba] alisema kwamba atatangaza kuhusu uzinduzi wa Ensaiklopidia Mpya ya Ahmadiyya iliyoanzishwa na '*Central Ahmadiyya Archive and Research Center*', Kituo kikuu cha Kumbukumbu na Utafiti cha Ahmadiyya. Watumishi wa kituo hiki walianza kufanya kazi kwenye mradi huu muda fulani uliopita, na sasa tovuti hii inapatikana kwa faida ya wanajamaat wote. Tovuti inayozinduliwa ni ***https://www.ahmadipedia.org*** ambapo kuna injini ya utafutaji ambayo inawezesha taarifa mbalimbali kutafutwa kwa urahisi. Matokeo ya utafutaji yatajumuisha 'viunganishi' (links) kwenye wavuti mbalimbali za Jumuiya, na video zinazohusika n.k. Pia kuna chaguo kwenye wavuti hii ambapo watu wanaweza kutuma matukio au taarifa za kihistoria ambazo wanaweza kuwa nazo ambazo hazijarekodiwa hapo awali. Baada ya uthibitishaji, taarifa hizi zitajumuishwa kwenye wavuti, na hivyo kuifanya iwe mradi ambao utaendelea kwa msaada wa wanajamaat wote wa Ahmadiyya. Ikiwa mtu yeyote hawezi kupata nyenzo au habari kwenye wavuti, mtu anaweza kuwasiliana na timu kuu, na watafanya kazi ya kutafuta na kufanya habari hiyo ipatikane. Idara kuu ya IT na wabashiri katika Kituo cha Kumbukumbu na Utafiti wamefanya kazi kubwa katika kuandaa nyenzo za wavuti hii.

Khalifa mtukufu[atba] aliwaombea wote waliohusika, na akasema kwamba baada ya sala ya Ijumaa, atazindua tovuti hii.



KITABU KIPYA

Mwanzo wa Mifarakano Ndani ya Islam

Islam Mein Ikhtilaafaat Kaa Aaghaaz (*Mwanzo wa Mifarakano Ndani ya Islam*) ni hotuba ya Kiurdu iliyotolewa na Hadhrat Mirza Bashir-ud-Din Mahmud Ahmad[ra], Khalifa wa pili wa Masihi Aliyeahidiwa[as]. Kusudi la msingi la hotuba hii lilikuwa kutoa maelezo sahihi na angalifu ya kihistoria ya mizozo ambayo iliibuka sana wakati wa *Ukhalifa* wa Hadhrat Uthman[ra].

Katika hotuba hii Hadhrat Mirza Bashir-ud-Din Mahmud Ahmad[ra] ameangazia maisha ya Hadhrat Uthman[ra], uchamungu wake na utawa, na hadhi yake mbele ya Mtukufu Mtume[saw]. Zaidi, ameelezea juu ya utakatifu wa masahaba wa Mtukufu Mtume[saw] na ameelezea jinsi mizozo ilivyotokea wakati wa mwanzo wa Islam. Kwa kuongezea, amekanusha madai kadhaa yaliyobambikwa dhidi ya Hadhrat Usman[ra] na wenzake.

Hotuba hiyo ni kito cha kitaaluma cha usomi na inaelezea matukio ya enzi ya *Ukhalifa* wa tatu kwa njia ambayo hakuna mwanahistoria mwingine aliyeweza kulinganisha, iwe ni Muislamu au sio Mwislamu; haya yote yamefanywa kwa ufasaha, kisomi, lakini kwa njia rahisi, kwa njia ya hadithi ya kupendeza.

Jipatie nakala yako kwa bei ya maktaba ya Tsh. 3,000/=

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

mapenziyamungu36@gmail.com